

Ulinganishi wa mofolojia na sintaksia baina ya lugha 19 za Kibantu za Afrika Mashariki

Hannah Gibson, Gastor Mapunda, Lutz Marten na Julius Taji

Ikisiri

Katika makala hii tumewasilisha matokeo ya utafiti wetu kuhusu lugha 19 za Kibantu za Afrika Mashariki. Tumeonesha kwamba kuna makundi makuu matatu ambayo yanafanana kiasi cha asilimia 70 au zaidi. Makundi haya yanajikuta katika maeneo mbalimbali ya eneo la utafiti wetu. Kuna kundi la kaskazini, la kati, na la kusini. Tumetumia mbinu maalumu ya kulinganisha mofolojia na sintaksia za lugha hizi, ambayo inatumia vigezo 142 kuelezea kiwango cha ufanano kati yao. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba kuna tofauti kubwa baina ya lugha hizi. Kiwango cha ufanano baina lugha hizi ni kati ya asimilia 45 (yaani uhusiano baina Kikuyu na Kisena) na 80 (baina Kiwabo na Kimakhuwa). Ili kufahamu kwamba kuna makundi maalumu miongoni mwa lugha hizi, tumegawanya lugha ambazo ufanano wao ni chini ya asimilia 70 na zile ambazo ufanano wao ni juu ya asimilia 70. Inawezekana kwamba uhusiano uliopo kati ya makundi haya unaonyesha uhusiano wao wa kihistoria.

1.0 Utangulizi

Makala hii inaelezea kiwango cha mfanano na tofauti katika mofolojia na sintaksia baina ya lugha 19 za Kibantu za Afrika Mashariki. Lugha ambazo zimehusishwa katika utafiti huu zinajumuisha Kinyole (E35), Kikuyu (E51), Kirombo (E623), Kidigo (E73), Kibende (F12), Kirangi (F33), Kimbugu (G221KK), Kiswahili (G42), Kindamba (G52), Kinyarwanda (JD61), Kifuliiru (JD63), Kiha (JD66), Kinyoro (JE11), Kiganda (JE15), Kimatengo (N13), Kisena (N44), Kiyao (P21), Kimakhuwa (P31) na Kiwabo (P34). Tunalinganisha lugha hizi kwa kutumia vigezo 142 vinavyohusisha sehemu maalumu za mfumo wa sarufi. Taarifa zipatikanazo kwa jinsi hiyo zinaingizwa moja kwa moja kwenye kanzi data maalumu iliyoandaliwa kwa ajili ya utafiti huu (Marten na wenzake, 2018).

Matokeo ya utafiti wetu yanaonesha kwamba, kwa upande mmoja lugha hizi zinafanana kisarufi, lakini kwa upande mwingine zinatofautiana kwa kiasi kikubwa. Kama tutakavyojadili zaidi katika makala hii, kuna makundi matatu ya lugha ambayo lugha zake zinaweza kutofautiana baina ya lugha za makundi hayo. Makundi haya yana lugha kati ya mbili hadi tano, na kila kundi linapatikana katika eneo lake la kijiografia katika utafiti huu. Katika utafiti huu, maeneo hayo ni kaskazini, eneo la kati, na eneo la kusini.

Utafiti huu unasaidia kuelezea kiwango cha ufanano na pia tofauti baina ya lugha za Kibantu za Afrika Mashariki. Kwa hiyo, inajikita katika kuelezea uhusiano uliopo kati ufanano wa lugha hizo kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine, utofauti wa maneno baina ya lugha hizi katika maeneo ambamo zinazungumzwa.

2.0 Usuli

Utafiti huu unahusisha lugha 19 za Kibantu zinazozungumzwa katika eneo la Afrika Mashariki, hasa katika nchi za Kenya, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na Uganda. Katika uanishaji wa lugha za Kibantu uliofanywa na Guthrie (1967-71) na Maho (2003), lugha hizi zinapatikana katika maeneo E, F, G, JD/JE, N na P. Orodha ya lugha hizo inaonekana katika Jedwali Na. 1:¹


Jedwali Na. 1: Lugha 19 za Utafiti huu

Msimbo wa Lugha	Jina la Lugha	Nchi Inakozungumzwa
E35	Kinyole	Kenya, Uganda
E51	Kikuyu	Kenya
E73	Kidigo	Kenya
E623	Kirombo	Tanzania
F12	Kibende	Tanzania
F33	Kirangi	Tanzania
G221KK	Kimbugu	Tanzania
G42	Kiswahili	Kenya, Tanzania
G52	Kindamba	Tanzania
JD61	Kinyarwanda	Rwanda
JD63	Kifuliiru	Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
JD66	Kiha	Tanzania
JE11	Kinyoro	Uganda
JE15	Kiganda	Uganda
N13	Kimatengo	Tanzania
N44	Kisena	Msumbiji
P21	Kiyao	Malawi, Msumbiji, Tanzania
P31	Kimakhuwa	Msumbiji
P34	Kiwabo	Msumbiji

¹ Lugha ya Kimbugu inajulikana kama lugha mchanganyiko, ambayo msimati wake unatoka katika lugha za Kikushitiki, lakini asili ya sarufi yake ni ya Kibantu. Tena, kuna lahaja mbili za lugha hii – lahaja ya ndani na ya kawaida. Lahaja ya ndani hutumika katika nyakati na miktadha maalumu, na hii nyingine ya kawaida ndiyo inayotumika kila siku katika jamii ya Wambugu. Katika makala hii tunatumia lahaja ya kawaida (kwa hiyo tunatumia G221KK) (angalia Mous 1994).

Ramani ifuatayo inaonesha maeneo ambayo lugha hizi zinazungumzwa:

Ramani Na. 1: Lugha 19 Zilizohusika katika Utafiti



Katika utafiti huu, tunatumia mtazamo maalumu ili kulinganisha mofolojia na sintaksia za lugha ambazo tunaziangalia. Mtazamo huo unafuata mfumo ulioandaliwa na Marten na wenzake (2007) na kufundishwa na wanazuoni wengine kama vile Petzell na Hammarström (2013), na Zeller na Ngoboka (2015). Wanazuoni hawa wamebainisha vigezo ambavyo wanavitumia katika kulinganisha makundi ya lugha za Kibantu. Katika utafiti huu tunaungana na Guérois na wenzake (2017) ambao wametumia vigezo 142 kulinganisha lugha zipatazo 50. Tunatumia tarifa zake, lakini kwa lugha 19 za Afrika Mashariki, Jumhuriya ya Kidemokrati ya Kongo na Msumbuji, kama zilivyoorodheshwa hapo juu.

Kuna historia ndefu ya kulinganisha lugha za Kibantu kama vile utafiti uliofanywa na Meinhof (1906). Baada ya hapo kulikuwa na kazi mbalimbali ziliyolinganisha sehemu maalumu za sarufi za lugha za Kibantu kama vile vimahali na upinduzi wa kimahali (Grégoire's 1975, Brenan na Kanvera 1989, Marten 2006, Khumalo 2010), vishazi rejeshi (Nsuka Nkutsi 1982, Zeller 2004, Henderson 2006) aliyelinganisha vishazi rejeshi. Hivi karibuni wanazuoni walianza kutumia mbinu maalumu ya kulinganisha lugha za Kibantu – kwa kutumia vigezo. Ingawa mbinu hiyo inatumiwa na wanazuoni wengi kuzingatia lugha za familia mbalimbali, na siyo lugha za Kibantu tu.

Vigezo vyenyewe vinahusisha sifa za kimofolojia kama vile ngeli za nomino, na sifa za kisintaksia, kama vile sentensi zenye yambwa mbili. Vigezo hivyo 142 ambavyo vimetumika vimegawanyika katika sehemu kumi na mbili ambazo zinatofautisha sehemu mbalimbali za sarufi, kama vile nomino na viwakilishi, unyambuaaji wa vitenzi, sentensi changamano, na kadhalika. Kila kigezo kinauliza swali kuhusu kuwepo au kutokuwepokwamuundo au tungo fulani katika lugha husika. Kwa mfano, kigezo namba sita kinauliza kama katika lugha husika hali ya udogo inadhihirishwa kwa kutumia ngeli fulani ya nomino. Orodha kamili ya vigezo hivyo inapatikana katika tovuti ya [http://bantu.soas.ac.uk/Guerois et al 2017 Parameters.pdf](http://bantu.soas.ac.uk/Guerois_et_al_2017_Parameters.pdf). Baada ya kukusanya taarifa zinazohusu vigezo vyote (au takribani vigezo vyote, tunajumuisha lugha ambazo tumepatazaidi ya asimila 80 ya taarifa), tunaweza kulinganisha lugha mbalimbali ili kujuani lugha zipi zinafanana zaidi kuliko nyingine, na pia lugha zipi ziko tofauti. Katika majadiliano yafuatayo tunatumia mtazamo huo na taarifa za lugha za Kibantu za Afrika Mashariki ili kuonesha uhusiano baina ya lugha hizo.

3.0 Matokeo

Matokeo ya utafiti huu ni ya aina tatu. Katika aina ya kwanza, tunatoa matokeo ya ulinganisho wa lugha zote kwa jumla. Kwa njia hii tunapata picha kamili ya uhusiano baina ya lugha zote zilizohusika katika utafiti huu. Katika aina ya pili, tunakokotoa wastani waulinganifu kati ya kila lugha na lugha nyingine zote tulizozifanyia utafiti. Katika aina ya tatu, tunaangalia kwa undani zaidi jinsi makundi haya matatu ya lugha yanavyojitokeza katika uchambuzi wetu.

3.1 Ulinganifu wa lugha zote

Matokeo yetu ya kwanza yanahusiana na ulinganifu wa lugha zote 19 za utafiti huu. Kwa kila lugha tumehesabu kiasi cha ufanano baina ya kila lugha na lugha nyingine zote. Kwa hiyo, tumepata asimila ya ufanano kwa kila lugha mbili zilizomo kwenye kanzi data. Matokeo ya lugha zote kwa ujumla yanaonekana katika Jedwali Na. 2:

	E35	E51	E623	E73	F12	F33	G221KK	G42-Ash	G52	JD61	JD63	JD66	JE11	JE15	N13	N44	P21	P31
E35																		
E51	63%																	
E623	61%	65%																
E73	57%	58%	66%															
F12	68%	60%	66%	62%														
F33	61%	64%	74%	65%	70%													
G221KK	65%	67%	71%	62%	70%	65%												
G42-Ash	57%	58%	58%	65%	65%	64%	66%											
G52	59%	58%	62%	58%	63%	71%	65%	67%										
JD61	66%	55%	54%	52%	61%	57%	58%	53%	57%									
JD63	64%	52%	51%	58%	66%	61%	56%	53%	56%	59%								
JD66	54%	55%	62%	68%	65%	63%	57%	58%	60%	58%	60%							
JE11	73%	59%	58%	60%	70%	64%	65%	57%	64%	67%	56%	61%						
JE15	74%	61%	57%	56%	61%	57%	61%	57%	60%	57%	58%	54%	72%					
N13	64%	51%	62%	55%	62%	57%	51%	49%	55%	54%	53%	49%	58%	53%				
N44	51%	45%	51%	55%	59%	56%	56%	62%	59%	51%	53%	62%	50%	54%	48%			
P21	56%	60%	57%	59%	67%	66%	60%	62%	61%	52%	54%	56%	62%	55%	63%	53%		
P31	54%	53%	55%	58%	61%	54%	62%	64%	51%	53%	53%	56%	58%	56%	52%	63%	54%	
P34	47%	48%	47%	56%	57%	50%	57%	60%	49%	46%	50%	58%	54%	52%	49%	62%	56%	80%

Tarifa ya Jedwali Na. 2 inaonesha kwamba tofauti kubwa zaidi kuliko zote ya asilimia ya ufananoni baina ya 45% na 80%. Uhusiano wa chini zaidi kuliko wote wa lugha mbili ni baina ya Kikuyu (E51) na Kisena (N44) kwa asilimia 45. Uhusiano wa lugha mbili wa juu zaidi kuliko zote ni baina ya Kimakhuwa (P31) na Kiwabo (P34) kwa asilimia 80. Kama inavyonekana katika Ramani Namba 1, lugha zote mbili za Kimakhuwa (P31) na Kiwabo (P34) zinazungumzwa katika nchi ya Msumbiji, na pia, maeneo ya lugha hizo yako jirani sana. Kwa upande mwingine, maeneo ya Kisena na Kikuyu yako mbali mno. Kisena kinazungumzwa katika Msumbiji na ni lugha ambayo inazungumzwa kusini kabisa katika lugha za utafiti wetu. Kikikuyu ni lugha ya Kenya na iko upande wa kaskazini, tofauti na msimamo wa Kisena. Kwa hiyo, tunaweza kuona kwamba ufanano na tofauti baina ya lugha hizi kwa kigezo cha sarufi kuna ufanano unaohusiana na umbali wao. Lugha za Kikikuyu na Kisena hazifanani sana, na umbali baina ya maeneo yao ni mkubwa. Hata hivyo, Kimakhuwa na Kiwabo zinafanana sana, na pia umbali baina ya maeneo yao ni mdogo.

Katika vipengele vifuatavyo tutaeleza matokeo mengine maalumu ambayo yanatokana na namna tulivyofanya ulinganifu.

3.2 Wastani wa ulinganifu

Jinsi nyingine kwa kufahamu uhusiano baina ya lugha za utafiti huu ni kwa kukokotoa wastani wa ulinganifu. Wastani wa lugha moja unahesabiwa kwa kujumlisha asilimia ya ufanano ya lugha moja na lugha zote nyingine, na kasha kugawanya jawabu na idadi ya lugha zote kwa jumla, lakini kwa kuondoa lugha moja (yaani 18). Matokeo ya kufanya hivi yanaoneshwa katika Jedwali Na. 3:

Jedwali Na. 3: Wastani wa Ulinganifu kati ya Lugha 19 za Afrika Mashariki

Msimbo wa lugha	Jina la lugha	Wastani
F12	Kibende	64%
F33	Kirangi	62%
G221KK	Kimbugu	62%
JE11	Kinyoro	62%
E35	Kinyole	61%
E623	Kirombo	60%
G42	Kiswahili	60%
G52	Kindamba	60%
E73	Kidigo	59%
JD66	Kiha	59%
P21	Kiyao	59%
JE15	Kiganda	58%
P31	Kimakhuwa	58%
E51	Kikuyu	57%
JD61	Kinyarwanda	56%
JD63	Kifuliiru	56%
N13	Kimatengo	55%
N44	Kisena	55%
P34	Kiwabo	55%

Data hizi zinaonesha kwamba lugha yenye wastani wa juu zaidi kuliko zote ni Kibende, ambacho kina wastani wa asilimia 64%. Kwa upande mwingine, Kimatengo, Kisena na Kiwabo ni lugha ambazo zina wastani wa asilima 55 na kwa hiyo, zina wastani wa mdogo zaidi kuliko zote.

Data zinaonesh pia kwamba, lugha nyingi ambazo zina wastani wa juu zinazungumzwa katika maeno ya kati au maeneo ya kaskazini. Kwa upande wengine, lugha nyingi zenye wastani wa chini zinazungumzwa upande wa kusini. Inaonekana kwamba lugha za kaskazini na za kati zinafanana zaidi kuliko zile za kusini.

Katika sehemu ifuatayo tutaeleza zaidi makundi matatu ambayo tumeshayataja katika utangulizi.

3.3. Makundi Matatu Maalumu

Matokeo ya utafiti wetu yanaonesha kwamba katika lugha hizi 19, kuna makundi matatu maalumu. Uhusiano baina ya lugha zilizomo ndani ya kundi moja ni zaidi ya asilimia 70, lakini uhusiano kati ya lugha za kundi moja na zile za kundi jingine

ni chini ya asilimia 70. Kila kundi linapatikana katika eneo maalumu la kijiografia – kundi moja liko kaskazini mwa eneo ambalo tumelifanyia utafiti, lingine liko kusini, na lingine liko katikati. Kila kundi lina lugha kati ya mbili na tano.


Kundi la kaskazini linajumuisha lugha tatu: Kinyoro (JE11), Kinyole (E35), na Kiganda (JE15). Jedwali Na. 4 linaonesha uhusiano baina lugha hizi tatu na lugha nyingine za ukanda wa E, yaani Kikuyu (E51), Kirombo (E623) na Kidigo (E73), na lugha nyingine za ukanda wa J, ni Kinyarwanda (JD61), Kifuliiru (JD63), na Kiha (JD66).

Jedwali Na. 4: Uhusiano kati ya Lugha za Kundi la Kaskazini na Lugha za Ukanda wa E na za Ukanda wa J

	E51	E623	E73	E35	JE11	JE15	JD61	JD63
E623	65							
E73	58	66						
E35	63	61	57					
JE11	59	58	60	73				
JE15	61	57	56	74	72			
JD61	55	54	52	66	67	57		
JD63	52	51	58	64	56	58	59	
JD66	55	62	68	54	61	54	58	60

Taarifa katika Jedwali Na. 4 inaonesha kwamba lugha za kundi la kaskazini, yaani Kinyoro (JE11), Kinyole (E35), na Kiganda (JE15), zote zina uhusiano zaidi ya asilimia 70 baina yao (lugha hizi pamoja na asilimia zao zinawekwa katika herufi nzito). Kwa upande mwingine, uhusiano baina ya lugha za kundi la kaskazini na lugha nyingine za ukanda wa E ni chini ya asilimia 70, na kwa baadhi ya lugha ni chini ya asilimia 60. Pia, uhusiano kati ya lugha hizi na lugha za ukanda wa JD ni kati ya asilimia 54 na asilimia 67. Kwa hiyo, tunaweza kusema kwamba kuna kundi moja la kaskazini linalojumuisha Kinyoro (JE11), Kinyole (E35), na Kiganda (JE15). Ramani namba 2 inaonesha eneo ambalo lugha za kundi hili zinapatikana, yaani eneo la kaskazini la utafiti wetu.

Ramani Na. 2: Lugha za Kundi la Kanda ya Kaskazini



Kama inavyooneshwa katika Ramani Na. 2, lugha tatu hizi za kundi la kaskazini zinazungumzwa upande wakasakazini kabisa mwa eneo la utafiti huu. Pia, maeneo ya lugha hizi ni jirani, na umbali kati yao ni mdogo. Vilevile, umbali wa maeneo na ufanano wa sarufi unafanana.

Katika mjadala wa isimu ya lugha za Kibantu kiulinganifu, matokeo yetu haya ni muhimu kwa sababu yanaonesha tofauti baina ya ukanda D, ukanda E, pamoja na ukanda J. Katika kazi yake ya kugawanya lugha za Kibantu katika kanda mbalimbali, Guthrie (1948, 1967-71) anatofautisha kati ya ukanda D na ukanda E. Hata hivyo, baada yamgawanyo wa Guthrie, wanazuoni wengine (taz. Bastin 2003) waliunda ukanda mwingine mpya, yaani ukanda J ambao unajumuisha baadhi ya lugha za

ukanda D na baadhi ya lugha za ukanda E. Wanazuoni hawa wanadai kwamba kuna uhusiano baina ya lugha za kanda hizi. Wanatumia hasa taarifa ya kifonolojia na kimofolojia kueleza maoni yao. Hata hivyo, matokeo ya utafiti wetu yanaonekana kutokukubaliana sana na uainishaji huu. Matokeo yetu yanaonesha kwamba kuna uhusiano wa kisarufi baina ya lugha tatu za ukanda E – haijalishi kama lugha husika imejumuishwa katika ukanda J (JE11, JE15) au haijajumuishwa (E35). Pamoja na ukweli huu, kwa upande mwingine, hayaoneshi uhusiano maalumu baina lugha nyingine za ukanda J (JD 61, JD63, na JD66), au zile za ukanda E (E51, E623, E73). Inaonekana kwamba uhusiano wa lugha hizi unafuata ujirani wa lugha hizi, badala ya kugawanya kanda D, E, au J. Pia, matokeo yanaonesha kwamba ufahamu wetu wa uhusiano baina ya lugha hizi bado haujakamilika na unahitaji utafiti zaidi.


Kundi la pili ambalo tumeliainisha katika utafiti wetu ni kundi la kati. Kundi hili linajumuisha lugha za Kirangi (F33), Kibende (F12), Kirombo (E623), na Kimbugu (G221KK). Uhusiano kati ya lugha hizi, pamoja na baadhi ya lugha za kanda JD, E, na G, unaoneshwa katika jedwali namba 5 (lugha za kundi la katikati, na asilimia zao zimepigwa chapa kwa herufi nzito).

Jedwali Na. 5: Lugha za Kundi la Kanda ya Kati na Lugha za Ukanda G

	JD66	E51	F33	F12	E623	G221KK	E73	G42
E51	55							
F33	63	64						
F12	65	60	70					
E623	62	65	74	66				
G221KK	57	67	65	70	71			
E73	68	58	65	62	65	62		
G42	58	58	64	65	58	66	65	
G52	60	58	71	63	62	65	58	67

Taarifa ya Jedwali Na. 5 inaonesha kwamba, uhusiano baina lugha nne za kundi hili ni asilimia 65 au zaidi, na wakati mwingine ni juu ya asilimia 70. Kwa upande mwingine, uhusiano wa lugha nyingine katika jedwali namba 5 siyo juu ya asilimia 68. Lakini jambo moja la pekee ni kwamba, uhusiano baina ya Kirangi (F33) na Kindamba (G52) ni asilimia 71. Lugha hizo nyingine za Jedwali Namba 5 zisizojumuisha kundi la kati, ni jirani za kundi la kati, kama inavyooneshwa katika Ramani Namba 2.

Ramani Na. 3: Lugha za Kundi la Kanda ya Kati



Ramani Na. 2 inaonesha maeneo ambapo lugha za kundi la kati zinazungumzwa. Lugha za kundi hili zinazungumzwa nchini Tanzania, baina ya lugha za Kenya na za eneo la Maziwa Makuu ambazo ziko kaskazini, na lugha za kusini mwa Tanzania, Msumbiji, na kusini mwa Malawi. Tena inaoneshwa kwamba lugha za Kiha (JD66), Kikikuyu (E51), Kidigo (E73), Kiswahili (G42), na Kindamba (G52) ni jirani za karibu zaidi za kundi hili. Kutokana na ukweli huo, tumeamua kuzijumuisha katika ulinganisho katika Jedwali Namba 5. Tofauti baina uhusiano baina lugha za kundi la kati na uhusiano baina jirani zao inaonesha uhalali wa kundi hili.

Mwishowe, kundi la tatu ni kundi la kusini linalojumuisha lugha mbili tu: Kimakuwa (P31) na Kiwabo (P34). Jedwali namba 6 linaonesha uhusiano uliopo baina ya lugha

hizi mbili na lugha nyingine za ukanda N na P, ambazo ni lugha jirani za kundi hilo – kama inavyooneshwa katika Ramani Na. 4.

Jedwali Na. 6: Lugha za Kundi la Kusini na za Kanda N na P

	N13	P21	P31	P34
P21	63			
P31	52	54		
P34	49	65	80	
N44	48	53	63	62


Ramani Na. 4: Lugha za Kundi la Kusini

Kundi la kusini ni kundi dogo ambalo linajumuisha lugha mbili tu. Hata hivyo, ni kundi lenye nguvu sana ambalo limejengwa na ufanano wa asilimia 80, ambao ni wa juu zaidi kuliko wa lugha zote zilizotumika katika utafiti huu. Tofauti na makundi mawili ya kaskazini na ya kati, kundi la kusini linafanana na kanda ya Guthrie (1967-71): lugha mbili za kundi la kusini zinajumuisha ukanda P na hasa kundi P30 katika ukanda huo. Kwa hiyo, eneo la uzungumzaji na uainishaji wa Guthrie (1967-71) hapa zinakubali.

4.0 Hitimisho

Katika makala hii tumewasilisha matokeo ya utafiti wetu kuhusu lugha 19 za Kibantu za Afrika Mashariki. Tumetumia mbinu maalumu ya kulinganisha mofolojia na sintaksia za lugha hizi. Mbinu hii inatumia vigezo 142 kuelezea kiwango cha ufanano kati yao. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba kuna tofauti kubwa baina ya lugha hizi. Kiwango cha ufanano kati ya lugha hizi ni baina ya asilimia 45 (yaani uhusiano baina Kikikuyu na Kisena) na 80 (baina ya Kiwabo na Kimakhuwa). Ili kufahamu kwamba kuna makundi maalumu miongoni mwa lugha hizi, tumegawanya lugha ambazo ufanano wake ni pungufu ya asilimia 70 na zile ambazo ufanano wao ni juu ya asilimia 70. Tumeonesha kwamba kuna makundi makuu matatu ambayo yanafanana kiasi cha asilimia 70 au zaidi yake. Makundi haya yanajikuta katika maeneo mbalimbali ya eneo la utafiti wetu. Kuna kundi la kaskazini, kundi la kati, na kundi la kusini.

Kundi la kaskazini linajumuisha lugha tatu ambazo zinasemwa katika nchi ya Uganda: Kinyoro, Kinyole na Kiganda (Kinyole kinaongelewa pia katika nchi ya Kenya). Mwiongoni mwa lugha za utafiti huu, hizi lugha tatu ni lugha pekee ambazo zinasemwa katika Uganda. Kwa hiyo inaonekana kwamba kiwango cha ufanano wao wa kimofolojia na kisintaksia unafanana na ujirani wao wa kijiografia.



Kundi la kati linajumuisha lugha za Kirangi, Kibende, Kirombo, na Kimbugu. Lugha zote hizo zinaongelewa nchini Tanzania, na hasa kaskazini mwa nchi hii, ila Kibende kinazungumzwa magharibi mwa Tanzania. Tukiangalia eneo kamili la utafiti wetu, lugha hizi zinatumiwa katika eno husika, kwa hiyo tumeliita kundi hili kundi la kati. Lugha mbili ambazo zimeungwa katika kundi la kusini ni Kimakhuwa na Kiwabo. Lugha hizi ni jirani kijografia, na zote mbili zinazungumzwa katika nchi ya Msumbiji. Makundi haya tuliyoyataja yanaonesha uhusiano baina ya lugha ambazo ziko jirani. Inawezekana kwamba uhusiano uliopo kati ya makundi haya unaonesha uhusiano wao wa kihistoria. Kwa upande mwingine, inawezekana kwamba unadhihirisha kuwepo kwa mchakato wa kuungana na ukopaji. Hata hivyo, utafiti zaidi unahitajika ili kufahamu vizuri matokeo ya hali tunayoishuhudia leo.

Shukrani: Tunawashukuru Peter Edelsten na Rozenn Guérois kwa msaada wa maoni na Leverhulme Trust Grant (RPG-2014-2018) kwa kugharimia utafiti wetu.

Marejeleo

- Bastin, Yvonne. (2003). "The Interlacustrine Zone". In D. Nurse and G. Philippson (eds.) *The Bantu Languages*. London: Routledge, 501-528.
- Guérois, Rozenn, Hannah Gibson and Lutz Marten. (2017). Parameters of Bantu Morphosyntactic Variation: Draft Master List. Alpha version, last amended 28 Dec 2017. Leverhulme Project 'Morphosyntactic Variation in Bantu: Typology, contact and change'. SOAS University of London
- Guthrie, Malcolm. (1948). *The Classification of the Bantu Languages*. London: Oxford University Press for the International African Institute (IAI).
- Guthrie, Malcolm. (1967/71). *Comparative Bantu: An Introduction to the Comparative Linguistics and prehistory of the Bantu languages*. London: Gregg International
- Maho, Jouni F. (2003). A classification of the Bantu Languages: An Update of Guthrie's Referential System. In D. Nurse and G. Philippson (eds): *The Bantu languages*, 639-51. London & New York: Routledge
- Marten, Lutz, Nancy C. Kula and Nhlanhla Thwala. (2007). 'Parameters of Morphosyntactic Variation in Bantu'. *Transactions of the Philological Society* 105:1-86.
- Petzell, Malin and Harald Hammarström. (2013). "Grammatical and Lexical Comparison of the Greater Ruvu Bantu languages". *Nordic Journal of African Studies* 22:129-57
- Zeller, Jochen and Paul Ngoboka. (2015). 'On Parametric Variation in Bantu, with Particular Reference to Kinyarwanda'. *Transactions of the Philological Society* 113:206-31.